

**TAARIFA KWA UMMA JUU YA USALAMA WA MAJI YA MITO
INAYOTIRIRIKA KUPITIA JIJI LA DAR ES SALAAM
KWENDA BAHARINI**

Ndugu Wananchi,

Ofisi ya Makamu wa Rais inapenda kutoa taarifa kwa umma juu ya juhudi za Serikali katika kuhakiki usalama wa maji ya mito jijini Dar es Salaam.

Kwa muda mrefu, taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na utafiti umefanyika juhudi mbalimbali katika kutuhakikishia usalama wa maji hayo, juhudi ambazo Ofisi yetu inapongeza kwa dhati.

Hata hivyo usalama wa hayo maji ni zoezi ambalo linatakiwa kuwa endelevu na linaotakiwa kuratibiwa na vyombo mbalimbali vya Serikali kupitia maelekezo ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Ili kufanikisha utaratibu huo, ofisi yetu kupitia Mhe. Naibu Waziri ilitembelea maeneo mbalimbali ya mito yetu na kuagiza vyombo mbalimbali vifanye uchunguzi na kuwasilisha taarifa kwa Mh. Waziri wa Nchi - Muungano na Mazingira.

Katika kufanikisha jambo hilo, tarehe 13/07/2017 Mh. Waziri wa Nchi - Muungano na Mazingira aliwaita watendaji wakuu wa vyombo husika na kufanya nao kikao juu ya njia muafaka ya kulifanya zoezi hilo.

Katika kikao hicho alisisitiza sana umuhimu wa kufuata taratibu za kisheria. Wote walikubaliana kwamba zoezi la uchunguzi wa kimaabara lifanywe kwa usimamizi wa Mkemia Mkuu wa Serikali katika maabara ya Serikali.

Timu ya wataalam mbalimbali imeanza kukusanya sampuli za maji ambazo zitawalishwa katika maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kupitia NEMC.

Tukipata matokeo na ushauri wa Mkemia Mkuu wa Serikali, tutajadili kama Serikali na hatua za kuchukuliwa zitaainishwa.

Tunaomba kuchukua nafasi hii kuwaomba wananchi na viongozi wao wawe watulivu wakati zoezi hili linafanyiwa kazi na wataalamu wetu ili kupata matokeo rasmi.

Aidha, taarifa zinazosambaa katika vyombo mbalimbali vya habari na mitandao ya kijamii ni ishara ya nia ya wananchi katika kupata ufumbuzi jambo ambalo litafanyiwa kazi na Serikali.

Imetolewa na:

Ofisi ya Makamu wa Rais

13/07/2017